Migawo ya mbele ya faida kufikia Shs.1.9 milioni ililipwa mnamo tarehe zilizotazamiwa. Migawo wa faida wa asilimia 15 (Shs.158 milioni) ulilipwa Wenye-hisa wa Kawaida waliosajiliwa katika vitabu vya Kampuni hii kufikia wakati wa kufunga biashara mnamo Aprili 8, 1998. Wakurugenzi wenu wanapendekeza mgawo wa mwisho wa faida wa pesa taslimu wa asilimia 25, ama Shs.5 kwa kila hisa, na kuunganisha Shs.264 milioni zaidi zitakazolipwa Wenye-hisa wa Kawaida waliosajiliwa katika vitabu vya Kampuni hii wakati wa kufunga biashara mnamo Novemba 18, 1998.

Kwa vile inahifadhi baadhi ya hisa, Serikali italipwa Shs.171 milioni kati ya jumla ya migawo ya faida iliyolipwa na itakayolipwa. Migawo hiyo pamoja na kodi inafanya mchango wa moja kwa moja kwa Serikali katika mapato ya kitaifa kuongezeka hadi Shs.3,809 milioni, ukiwa umeongezeka kutoka Shs.3,190 milioni mnamo 1996/97.

**TOLEO LA BAKSHISHI**

Wakurugenzi wameamua kutumia kiasi cha Shs.527,520,000 kutoka kwenye akiba ya mapato na kutoa kiasi hiki kama tolea la bakshishi kwenye hisa. Hisa mpya zitabadilishwa kama viungo vya hisa na kupeanwa kama hisa moja mpya ya Shs.20 kwa viungo viwili vya hisa. Ijapokuwa hisa hizi mpya zitapendekezwa katika mgawo wa mkutano mkuu ujao, hata hivyo, zitapendekezwa kwenye hisa zingine zote zilizoko kwenye kampuni. Pendekezo lifaalo litatolewa kwenye mkutano ujao wa mwaka.

**KUFANYIWA MAREKEBISHO KWA KIFUNGU NAMBARI 110**

Kifungu nambari 110 cha makampuni kinawapa wakurugenzi kiwango fulani cha uwezo kuhusiana na shughuli za kampuni, kukopa pesa ama kutoza kampuni pesa, mali na kutoa stakabadhi ya pesa zilizokopwa ama kutoa dhamana kwa deni lolote linalokopwa. Kiwango hicho cha uwezo hakiwezi kuzidishwa kabla ya kuidhinishwa na wenye hisa. Hii ina maana kwamba wakurugenzi hao ni sharti kwanza wapate idhini kutoka kwa wenye hisa wakati wa mkutano mkuu kabla ya kifungu hicho kufanyiwa marekebisho, ikiwa kiwango cha uwezo uliowekwa kimo kwenye hatari ya kukiukwa. Kifungu hicho kilifanyiwa marekebisho kwa mara ya mwisho mnamo mwaka wa 1990, wakati kiwango cha ukopaji kilipopandishwa hadi kufikia shillingi billioni 4, na kutokana na upanuzi wa haraka wa shughuli za kampuni, kifungu hiki kinahitaji kufanyiwa marekebisho.

Mashauri yamefanywa baina ya mawakili wa kampuni, wahasibu na soko la uzaji wa hisa la Nairobi ambao wana maoni sawa kwamba kiwango kama hicho cha uwezo ni cha juu mno kuhusiana na kampuni zinazohusika na ni pingamizi kuhusiana na shughuli za sasa za kibiashara. Kwa sababu hiyo kinapasa kuondolewa ili kuepusha marekebisho ya mara kwa mara ya kifungu hicho. Wakurugenzi wako wanakubaliana na wazo hilo, na wamependekeza kwamba kifungu hicho kifanyiwe marekebisho wakati wa mkutano mkuu wa kila mwaka wa kampuni ili kuondoa kiwango hicho.


...zote za mdundu kwa wateja, sasa zinayo huduma...  
kompyuta na makarans... kwenye mezi za mdundu...  
na za malipo. Topp... anaonekana akilipa billi yake...  
afisi ya huduma kwa wateja, Stima Plaza, Nairobi.

CMA-LIBRA

THE KENYA POWER & LIGHTING CO. LTD.

**MABADILIKO KWENYE SHUGHULI ZA UMEME**

Kufuatia utenganishaji wa kazi ya kutoa umeme kutoka usambazaji na ugawaji chini ya mabadiliko ya sekta ndogo ya umeme, kampuni moja ya ushauri wa kitaalamu, Price Waterhouse nchini Uingereza, iliteuliwa na Serikali kufanya utafiti wa kukadiria thamani ya rasilmali. Utafiti huu unahusu ukadiriaji wa thamani ya rasilmali zitakazohamishwa kati ya Kenya Power and Lighting Company (KPLC) na Kenya Electricity Generating Company Ltd. (KenGen) ambayo zamani ilikuwa Kenya Power Company Ltd. Chini ya mabadiliko hayo, KPLC itamiliki rasilmali za usambazaji na ugawaji, ilhali KenGen itamiliki rasilmali za kutoa umeme. Mapendekezo ya mwisho ya ripoti kuhusu mabadiliko hayo tayari yamewasilishwa na yanachunguzwa.



*Mitambo ya Kompyuta imewekwa kote nchini kwa nia ya kuhudumia wateja vyema zaidi: Wasoma mita wakitumia mitambo ya kompyuta ya kushika kwa mkono inayotumika kusoma mita kwa urahisi.*

Serikali imeteua pia kampuni nyingine ya ushauri, Merz and McLellan nchini Uingereza kurekebisha utafiti wa orodha ya malipo ya umeme ya 1993 na kupendekeza orodha ya malipo ambayo yatumika kwenye sekta hii iliyobadilika. Pamoja na hayo, Serikali iliteua wanachama wa Halmashauri ya Usimamizi wa Umeme (ERB), iliyoundwa chini ya Sheria ya Umeme, 1997, ambayo wajibu wake, miongoni mwa maswala mengine, ni usimamizi wa orodha ya malipo ya umeme.

**MRADI WA UIMARISHAJI WA HUDUMA (ISP)**

Kwa kutilia mkazo uridhishaji wa wateja, Mradi wa Uimarishaji wa Huduma (ISP), uliendelea kunufaisha huduma za kampuni hii kupitia kwa mpango wa kutumia kompiuta ambao tayari umetekelezwa. Chini ya mradi huu, Kampuni hii imeimarisha huduma zake kwa kutoa wakati unaohitajika takwimu za usimamizi wa shughuli zake, na hivyo, kuweka msingi imara wa maendeleo ya sasa na siku zijazo. Chini ya mradi huo, Kampuni hii, katika miaka mitatu iliyopita, imeanzisha kituo cha kisasa cha kompiuta katika Stima Plaza, kuunganisha mawasiliano ya mitambo ya kompiuta kote nchini, na kuwapa mitambo ya kisasa na ustadi wafanya kazi wake kupitia mipango mbali mbali ya mafunzo.

Mbali na haya, huduma zote muhimu ikiwemo ni pamoja na usomaji mita, hati za kudai malipo, ukusanyaji pesa, huduma za dharura, maombi ya huduma mpya za umeme, uhasibu, mpango wa matibabu ya wafanya kazi (Medicare) na utayarishaji mishahara zimeimarishwa zote ili kutoa huduma za haraka. Mitambo hiyo ya kompiuta inayotumiwa na kusimamiwa na wataalamu wa Kampuni, imeratibishwa kutumiwa hadi kupita mwaka wa 2000 (Y2K).

Kama sehemu moja muhimu ya kuonyesha mfano mwema wa uthabiti na ustaarabu, tuliendelea kubadilisha upya huduma za wateja afisini, mavazi ya wafanya kazi, mbao za matangazo na vifaa vingine vya kujitambulisha vya Kampuni hii.

Mradi huu, ambao sasa unapigwa msasa zaidi, upo katika awamu ya mwisho ya ushirikishaji, utekelezaji na usimamizi.

**HUDUMA KWA WATEJA**

Kuambatana na shabaha muhimu ya Kampuni hii ya kuimarisha zaidi natija ya huduma kwa wateja wetu, Kampuni hii ilianzisha Idara ya Huduma kwa Wateja na pia kuimarisha zaidi ukusanyaji mapato. Huduma hii inahusisha utayarishaji wa maombi ya huduma mpya za umeme, usomaji mita, ukusanyaji mapato, kufungua na kufunga akaunti, uhusiano na wateja na uzaji. Afisi zetu zote kuu za huduma kwa wateja sasa zinatoa huduma kupitia kompiuta katika kaunta za kuwasilisha maswali na malalamiko.

Pamoja na hayo, mitambo mingine ya kompiuta yenye lengo la kuimarisha zaidi huduma kwa wateja pia inatumiawa katika afisi zote za Kampuni hii. Hii ni pamoja na mitambo ya kompiuta ya kutayarisha maombi ya huduma mpya za umeme (ICS) na usimamizi wa huduma zote kwa wateja; Mitambo ya Kompiuta za Uchoraji na Ujenzi (DCS) wa waya zote za ugawaji na vituo vidogo; na Mitambo ya Kompiuta za Huduma za Dharura

(IMS) na shughuli nyingine za kawaida za mpangilio wa ugawaji. Utumiaji wa mitambo hii umesaidia katika kuimarisha zaidi natija ya huduma kwa wateja.

Katika afisi za Huduma za Dharura, vituo vipya vya kupokea simu vilianzishwa ambapo simu zinazopokewa zinaratibishwa kwa kompiuta na kuwasilishwa papo hapo kwa mitambo ambayo inasimamia shughuli za mafundi wa umeme. Hii imesaidia kupunguza muda mrefu unaotumiwa kushughulikia simu za huduma za dharura zinazopokewa kutoka kwa wateja.

Ili kusaidia katika kuharakishia wateja huduma za kupokea malipo ya huduma za umeme, matayarisho yanafanywa kuongeza afisi zaidi za malipo hasa mjini Nairobi.

## USAMBAZAJI NA UGAWAJI

Kufuatia mabadiliko kwenye sekta ndogo ya umeme, Kampuni yenu ilihifadhi wajibu wa usambazaji na ugawaji umeme. Katika wajibu huo, Kampuni hii hununua umeme kutoka kwa KenGen na Independent Power Producers (IPPs) ili kuuzia wateja wake.

Ili kutimiza lengo hili, Kampuni hii inatilia mkazo juhudi zake katika miradi ya usambazaji na ugawaji pamoja na mipango ya uimarishaji na usimamizi.

### *Maendeleo ya Usambazaji, Mipango ya Uimarishaji na Usimamizi*

Miongoni mwa miradi iliyopendekezwa chini ya Least Cost Development Plan, iliyotekelezwa na Kampuni hii ikisaidiwa na Acres International, ni pamoja na waya za usambazaji za Kiambere-Nairobi 220kV na Kipevu-Rabai 132kV.

Kampuni nyingine, Mott MacDonald, iliteuliwa washauri wa utayarishaji wa hati za zabuni na ukaguzi wa utekelezaji wa miradi hiyo yote miwili. Zabuni za ujenzi wa waya hizo tayari zimealikwa na miradi hiyo inatazamiwa kuanza kufanya kazi rasmi mnamo 2000.

Kampuni hii iliimarisha zaidi kote nchini mpango wa ugawaji umeme na uimarishaji na usimamizi wa huduma zake ili kukuza zaidi uthabiti na upokezi wa umeme wakati wote. Hii itapunguza hitilafu za mara kwa mara na ukatizaji wa huduma za umeme.

Mjini Nairobi, Shs.208 milioni zilitumiwa katika kuanzisha kituo kidogo kipya 66/11kV katika Kileleshwa na kupandisha hadhi kituo kidogo cha Parklands kutoka 42MVA hadi 90MVA.


Kiasi kingine cha Shs.93 milioni kilitumiwa katika miradi mitatu ya uimarishaji huduma katika Nyali, Malindi na Kipevu katika Mkoa wa Pwani na kingine cha Shs.89 milioni kikatumiwa katika Kenya Magharibi. Kiasi kingine cha Shs.45 milioni kilitumiwa katika uimarishaji huduma katika maeneo ya Mlima Kenya, Rift Kati na Rift Kaskazini. Kampuni hii pia iliimarisha zaidi usimamizi wa mpango wa ugawaji kuhusu ubadilishaji wa transfoma zilizozidiwa na matumizi, milingoti iliyooza, waya zilizofifia, ufyekaji, miongoni mwa mipango mingine, na pia usimamizi wa vituo vidogo vya umeme.

Usimamizi wa mpangilio wa waya za usambazaji bila kukatiza umeme uliimarishwa pia kwa kutumia helikopta ya Kampuni hii.

### *Upunguzaji wa Upoteaji wa Umeme na Mahitaji ya Mipango ya Kuhusika ya Usimamizi*

Kampuni hii imeanzisha Mpango wa Kupunguza Upoteaji wa Umeme utakaogharamiwa chini ya fadhili ya International Development Association (IDA). Pia kugharamiwa chini ya fadhili hiyo ni mpango wa kuhusisha wateja kwenye usimamizi wa umeme na uhifadhi wa nishati. Mipango hii miwili inatazamiwa kuendelea kuanzia 1998 hadi 2003 na uteuzi wa wataalamu washauri kusaidia katika utekelezaji wao unakaribia kukamilika.

**FAIDA KABLA YA KULIPA KODI** MABILLIONI (SRS).



**UIMARISHAJI WA UWEZO WA UTOAJI UMEME**

**Mitambo ya kuongezea huduma zaidi za umeme**

Mitambo miwili hasa, Iberafrica Power (Kenya) Ltd. katika Nairobi South na Westmont Power (Kenya) Ltd. katika Mombasa, yenye uwezo wa kutoa 88MW za umeme, iliendelea kutimiza wajibu wao kwa hali ya kuridhisha na kuongezea sana huduma zaidi za umeme, hasa wakati mtambo wa 72.5MW wa Kituo cha Umeme cha Gitaru ulipofungwa kwa muda mrefu baada ya kutokea hitilafu ya transformo.

*Uwezo wa kutoa umeme unakusudiwa kuimarishwa zaidi kwa 533MW katika muda wa miaka mitano ijayo, kutokana na utekelezaji wa miradi ifuatayo katika sekta ya umma na binafsi:*


**Mtambo wa Gesi wa 30MW**

Katika Kipevu, mtambo wa gesi wa 30MW, ambao kwa wakati huu unakaribia kukamilika nchini Uingereza, unatazamiwa kuanza kufanya kazi tena mnamo Machi, 1999.

**Miradi ya haraka ya utoaji umeme**

Wakati wa Mpango wa Least Cost Development Plan, ilithibitishwa kwamba mitambo miwili ya 55MW kila

**IDADI YA WATEJA**



moja, inahitajika haraka iwezekanavyo kupunguza upungufu wa umeme unaotazamiwa kutokea hadi miradi inayohusika ya kuimarisha zaidi utoaji umeme itakapoanza kutumiwa. Kadhalika, ilipendekezwa kwamba ili kuhakikisha usawa na uthabiti katika huduma, mtambo mmoja uwe Eldoret, na mwingine Nakuru. Makampuni ya binafsi (IPPs) tayari yamewasilisha maombi na ukadiraji umekamilika. Maombi ya mapendekezo pia yamepelekewa makampuni yaliyoorodheshwa na zabuni zinatazamiwa kuwasilishwa kufikia mwishoni mwa 1998. Mitambo hiyo inatazamiwa kuanza kutumiwa 2000.

**Mradi wa pili wa Kipevu wa MW 75**

Kandarasi ya kustawisha mradi huu ilipewa kampuni ya Wartsila NSD Power Development na makubaliano ya kununua umeme yame-tekelezwa. Mradi huu unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa 2000.

**Kituo cha tatu cha Oikaria**

Mashauriano bado yanaendelea na Ormat International Inc. Mkataba wa Ununuzi wa Umeme umetekelezwa na wastawishaji, na kazi muhimu za mwanzoni zimeanzishwa. Mitambo huu unatazamiwa kukamilika 2002.

**Miradi ya KenGen**

KenGen imeanza kutekeleza miradi minne inayogharimiwa na umma ya kutoa umeme jumla ya 254MW. Hii ni: mtambo wa tatu wa 72.5MW wa Gitaru, mtambo wa kwanza wa dizeli wa 75MW wa Kipevu, mtambo wa pili wa 64MW Oikaria, wa huduma za umeme kutokana na mvuke na mpango wa umeme wa kutokana na maji wa 60MW wa Sondu Miriu. Miradi hii inatazamiwa kukamilika wakati mbali mbali kufikia 2002.

**UMEME KATIKA MASHAMBANI**

Kwa niaba ya Serikali, Kampuni yenu iliendelea na utekelezaji wa mipango ya upelekaji umeme katika sehemu za mashambani. Katika mwaka huo, Shs.454 milioni zilitumiwa katika upanuzi wa waya za umeme kwa mipango 620 ambayo ilikuwa katika viwanda mbali mbali vya utekelezaji na kufanya gharama zao kwa jumla kufikia Shs.3,368 milioni tangu ianze kutekelezwa.

Idadi ya wateja chini ya mipango hiyo iliongezeka kwa 2,736 ama asilimia 5 kutoka 55,242 hadi 57,978. Vimo vya umeme vilivyouzwa viliongezeka kutoka 150 milioni hadi 153 milioni, ongezeko la asilimia 2. Mapato yalifikia Shs.864 milioni ikilinganishwa na Shs.849 milioni katika mwaka uliotangulia, ongezeko la asilimia 2.

Serikali ya Kenya na Tume ya Jumuiya ya Ulaya zilitia sahihi mkataba wa kutenga Shs.375 milioni kutoka kwa hazina za Thibiti ya Mauzo ya Kigeni (STABEX) kugharimia awamu ya kwanza ya Mpango wa Usambazaji wa Umeme katika Viwanda vya Kahawa vya Sehemu za Mashambani (COFREP). Mpango huo unakusudiwa kuimarisha zaidi uthabiti na natija ya utayarishaji kahawa kwa kubadilisha mitambo ya dizeli na ile ya kuendeshwa na umeme. Awamu ya kwanza ya mpango huo inalenga viwanda 168 vya kahawa kote nchini. Kufikia sasa, Shs.120 milioni zimetolewa kuweka umeme katika viwanda 57 kama hivyo vya kahawa.



*Mitambo ya kompyuta iliowekwa kote nchini imesaidia sana kurahisisha huduma kwa wateja. Hapa, wafanyakazi wana-jaribu mtambo wa kompyuta ambao umekamilika karibuni.*

Viwanda 20 na maombi mengine ya umeme ya viungani mwao vilipelekewa umeme katika mwaka huo na shughuli za upelekaji umeme kwenye viwanda vingine 37 ziko kwenye viwango mbali mbali za utekelezaji.

Kufuatia uanzishaji wa Hazina ya Umeme Mashambani chini ya Sheria ya Umeme, 1997, kodi ya asilimia 5 inalipishwa mauzo yote ya nishati ya umeme kutoka kwa Kampuni hii. Hii itasaidia kuimarisha zaidi Hazina ya Umeme Mashambani kwa kuongezea Shs.600 milioni mwaka huu na kuwezesha wateja zaidi kupelekewa huduma za umeme nchini.

## WAFANYA KAZI NA MAFUNZO

Tunaendelea kutilia mkazo wajibu unaotekelezwa na wafanya kazi katika kutimiza shabaha za Kampuni hii. Hivyo, katika mwaka unaoelezwa tuliimarisha zaidi umoja wetu kwa kushirikiana na kutekeleza madhamira yetu, wajibu na mwelekeo mpya wa Kampuni na wafanya kazi wetu. Hii ilifanywa kupitia kwa semina kadhaa na mijadala katika majukwaa mbali mbali. Juhudi hizo pamoja na motisha zilizoendelea pamoja na maslahi ya wafanya kazi wetu kupitia malimbikizo ya kuvutia na mipango ya mafunzo, zilichangia sana katika kuimarisha zaidi huduma kwa wateja na matokeo ya biashara.

Jumla ya Shs.133 milioni zilitumiwa katika mafunzo ya jumla ya wafanya kazi 4,578 katika Chuo cha Mafunzo cha Kampuni hii na taasisi nyingine. Kati ya kiasi hicho, Shs.46 milioni zilitumiwa katika mipango muhimu ya mafunzo na maendeleo ya usimamizi, teknolojia takwimu, afya na usalama kazini, huduma kwa wateja na maendeleo ya ufundi. Mipango hii ilifanywa hapa nchini na ng'ambo.

Kwa kutambua umuhimu wa uelewano kazini katika kuimarisha zaidi uzalishi, Kampuni hii ilidumisha ushirikiano wa manufaa na viongozi wa wafanya kazi (KETAWU) katika maswala yote kuhusiana na maslahi yao na, hivyo, kuhakikisha amani na ushirikiano kote katika mwaka huo.


Kampuni hii ilikuwa na wafanya kazi 7,167 kufikia Juni 30, 1998, ikilinganishwa na wafanya kazi 8,279 katika mwaka uliotangulia. Katika mwaka unaoelezwa, wafanya kazi 1,591 waliondoka ikilinganishwa na wafanya kazi 311 katika mwaka uliotangulia. Kati ya hao, wafanya kazi 1,390 waliamishwa hadi KenGen chini ya mpango wa mabadiliko ya sekta ndogo ya umeme, ilhali wengine waliondoka kwa sababu za kawaida. Kiwango cha wateja wanaotumikiwa na wafanya kazi kilifikia 63:1 ikilinganishwa na 51:1 katika mwaka uliotangulia.

## UHUSIANO NA UMMA

### Mawasiliano na Elimu ya Wateja

Katika mwaka unaoelezwa, Kampuni hii iliendelea kuhimiza elimu ya wateja pamoja na kuimarisha sifa yake. Kama sehemu ya juhudi zilizodumishwa za kuwafikia wateja na wananchi kwa jumla, Kampuni hii ilishiriki katika Maonyesho 11 ya Chama cha Kilimo nchini Kenya (ASK), na ikajishindia zawadi 30 za kwanza, tano za pili na sita za tatu katika mashindano mbali mbali ya maonyesho hayo. Vibanda vyetu vipya vya maonyesho katika Nairobi, Mombasa na Nakuru, pamoja na mapambo yao na utumiaji wa mbinu za kisasa za maonyesho, vilichangia katika matokeo hayo mazuri. Vifaa hivyo vilivyoimarishwa pia vilisaidia Kampuni hii kuonyesha kikamilifu huduma zake na bidhaa na kuridhisha wananchi waliotembelea vibanda vyake. Habari kuhusu shughuli za Kampuni hii na huduma kwa wateja, historia, uhifadhi wa umeme na usalama pia zilisambazwa katika maonyesho hayo.

## UZALISHAJI KULINGANA NA KIINI



- ▶ Nguvu za maji
- ▶ Nguvu za mvuke
- ▶ Wazalishaji wa kibinafsi (IPP)
- ▶ Mvuke
- ▶ Halmashauri ya umeme ya Uganda (UEB)

Filamu mpya kuhusu maendeleo ya Kampuni hii na wajibu ilitayarishwa na kuonyeshwa katika televisheni ya Shirika la Utangazaji la Kenya (KBC) na mashirika mengine na kupitia filamu za kuonyeshwa uwanjani. Filamu hiyo, "Future Current", itaendelea kuonyeshwa kupitia majukwaa mbali mbali nchini na ng'ambo.



*Mkurugenzi mkuu Bw. S.K. Gichuru, anapeana hundi kusaidimakao ya watoto ya Dr. Barnados.*

Shughuli za Kampuni hii na miradi yake zilitangazwa kupitia magazetini, televisheni na radioni ilhali kipindi cha radioni, "Ulimwengu wa Reddy Kilowatt", kiliendelea kuwa kielelezo muhimu cha kuwafunza wananchi na kutangaza Kampuni hii.

Wateja waliendelea kuelimishwa kupitia filamu, taarifa za habari, makala ya Kampuni hii, "Stima Newsletter", makala mbali mbali, matangazo, vituo vya ushauri wa wateja na kupitia mbinu tofauti za utangazaji masokoni na shuleni.

Stima Newsletter ilichapishwa mara kwa mara kujulisha wafanya kazi na wahusika wengine shughuli na miradi ya Kampuni hii.

### **Ufadhili kwa Jamii**

Kama Kampuni inayojitambulisha na uzalendo na ukarimu, Kampuni hii ilidhamini mipango mbali mbali ya ufadhili katika mwaka huo. Pesa zilipewa makao ya watoto ya Dr. Barnardos na Dagoretti na Hospitali ya Wagonjwa Wasiotibika ya Eldoret. Wafanya kazi walichangisha pesa kusaidia wagonjwa wa maradhi ya moyo kwa kushiriki katika Dettol Heart Run na Kampuni hii pia ilipatia vitabu na kuanzishia Starehe Boys Centre Hazina ya Elimu ambapo wanafunzi wawili wa shule hiyo watakuwa wakilipiwa karo kila mwaka.

### **MATUMAINI YA SIKU ZIJAZO**

Ni jambo la kutia moyo kwamba katika kiwango cha kitaifa, wahusika muhimu wanashughulikia swala la kufufua uchumi. Serikali hasa imetangaza hatua mathubuti katika kupunguza gharama na kuimarisha uzalishi. Hii pamoja na mpango unaokusudiwa wa kupunguza watumishi wa umma, kuwepo kwa sekta changamoto ya binafsi, ari ya sekta zote muhimu katika kubadilisha Kenya kuwa taifa lenye maendeleo zaidi ya viwanda (NIC) kufikia 2020 na ufufuaji wa ushirikiano wa kanda hili, itasaidia katika kufufua haraka uchumi na kudumisha mwelekeo wa maendeleo.

Katika sekta ndogo ya umeme, vikwazo katika uwezo wa utoaji umeme, ambavyo vilitatiza mahitaji wakati uliopita, vinachunguzwa. Katika KPLC, tumejitolea mhanga na kuimarisha zaidi uwezo wetu katika kutekeleza ipasavyo wajibu wetu katika siku zijazo na kutimiza kamili wajibu wetu katika kudumisha mwendo wa maendeleo ya kitaifa.

Pia, ni habari njema kwamba kiwango cha ufanisi cha matumizi ya umeme miongoni mwa wateja wa kadiri wa biashara na viwanda mnamo 1997/98 kimeendelea kuimarika. Hii inadhahirika hasa katika viwanda vya mboga, matunda na maua ambavyo Kampuni hii imenufaisha sana kwa kuvipa umeme thabiti. Kadhalika, kuna matumaini ya nafasi zaidi za biashara hasa katika viwanda vya migodi na madini, hasa katika Mkoa wa Pwani ambapo kampuni moja kutoka Canada imepewa leseni ya kuchimba na kutayarisha madini ya *titanium*.

Mradi tu hatua za kufufua uchumi zifue dafu, kuna matumaini ya ongezeko zaidi katika mahitaji ya umeme, na kusaidia pia kuimarisha zaidi shughuli zetu. Ni muhimu, hata hivyo, kwamba tujiandae kujitolea zaidi katika kuimarisha usimamizi na faida katika nyanja za ukusanyaji mapato na matumizi ya pesa. Kwa kutambua wajibu huo, wakurugenzi wenu wamechukua hatua mathubuti ili kuweka Kampuni yenu katika barabara ya haraka ya kunufaika kamili na nafasi zinazotokea zaidi za biashara.

### **Shukrani**

Kwa niaba yenu na Halmashauri hii, napenda kuwashukuru wateja wetu wote, Serikali na vituo vyake, mashirika yanayotukopesha pesa, wasimamizi wetu wastadi na wafanya kazi wote kutokana na wajibu na michango yao katika kuleta matokeo ya kusifika ya biashara chini ya hali ngumu.

**Titus T. Naikuni**

**Mwenyekiti**

Oktoba 15, 1998



The directors submit their report together with the audited financial statements for the year ended 30<sup>th</sup> June, 1998.

### ACTIVITIES

The principal activities of the Company continued to be the distribution and sale of electricity from energy purchased from local bulk supply companies, the Company's own generating stations and the Uganda Electricity Board.

### RESULTS AND DIVIDENDS

	<b>Sh'000</b>
Profit before taxation	2,005,343
Provision for taxation	541,068
Profit after taxation	1,464,275
Preference dividends paid for the year on: 350,000 7% Cumulative Preference Stock units (gross)	490
1,800,000 4% Cumulative Preference Stock units (gross)	1,440
	1,930
Ordinary Stock dividends	422,016
	423,946
Retained profit for the year transferred to revenue reserves	1,040,329

### DIVIDENDS

An interim dividend of Shs.3 (15%) per share was paid on 30<sup>th</sup> April, 1998. The directors recommend payment of a final dividend of Shs.5 (25%) per share making a total dividend of Shs.8 (40%) per share for the year.

### CAPITAL EXPENDITURE

During the year, a total of Shs.2,683,396,000 was spent on fixed assets. Capital contributions received from customers amounted to Shs.1,141,205,000 resulting in a net capital cost to the company of Shs.1,542,191,000. Net capital work-in progress as at 30<sup>th</sup> June, 1998, amounted to Shs.1,898,924,000 compared to Shs.1,233,498,000 at the end of the previous year.

Wakurugenzi wanatoa taarifa yao pamoja na taarifa ya ukaguzi wa fedha kwa mwaka uliomalizika tarehe 30 Juni, 1998.

### SHUGHULI

Shughuli kuu za kampuni ziliendelea kuwa kusambaza na kuuza stima inayotokana na kawi iliyonunuliwa kutoka kwa kampuni za hapa nchini, vituo vyake yenyewe vya uzalishaji umeme na kutoka kwa halmashauri ya stima ya Uganda.

### MATOKEO NA MGAWO WA MAPATO

	<b>Sh.'000</b>
Faida kabla ya kulipa Ushuru	2,005,343
Tafaa la Ushuru	541,068
Faida baada ya kulipa Ushuru	1,464,275
Mgawo wa faida za hiari uliolipwa katika mwaka kwa: 350,000 7% Cumulative Preference Stock units (gross)	490
1,800,000 4% Cumulative Preference Stock (gross)	1,440
	1,930
Mgawo wa kawaida wa faida	422,016
	423,946
Faida iliobaki na kuhamishwa kwa mabaki ya mapato	1,040,329

### MGAWO WA MAPATO

Mgawo wa muda wa kati wa Shs.3 (15%) kwa hisa ulilipwa mnamo Aprili 30, 1998. Wakurugenzi wanapendekeza malipo ya mwisho ya mgawo na mapato wa Shs.5 (25%) kwa hisa. Ikijumlishwa inakuwa Shs.8 (40%) kwa kila hisa katika mwaka huu.

### MATUMIZI YA MALI

Katika mwaka, jumla ya Shs.2,683,396,000 zilitumiwa kwa mali thabiti. Kiasi cha pesa zilizopokelewa kutoka kwa wateja kilikuwa ni Shs.1,141,205,000 na kufanya gharama kwa kampuni kuwa Shs.1,542,191,000. Jumla ya kiasi cha matumizi kwa kazi inayoendelea kufikia Juni 30, 1998, kilikuwa Shs.1,898,924,000 ikilinganishwa na Shs.1,233,498,000 kufikia mwisho wa mwaka uliotangulia.

**DIRECTORS**

The present members of the board of directors are shown on page 2.

Mr D. O. Kombo resigned on 29<sup>th</sup> July, 1997.

Mr F. M. Nyaga was appointed a director on 17<sup>th</sup> December, 1997, and Ms M.K. Chemengich joined the Board on 13<sup>th</sup> March, 1998, following her appointment as Permanent Secretary in the Ministry of Finance in place of Mr S.S. Lesrima.

In accordance with Regulation 128 of the Articles of Association, Ms M. K. Chemengich retires and, being eligible, offers herself for re-election.

In accordance with Regulation 120 of the Articles, Mr S.O.J. Ambundo, Mr T. D. Owuor and Mr T. T. Naikuni retire and, being eligible, offer themselves for re-election.

**AUDITORS**

The auditors, Deloitte & Touche, having indicated their willingness, continue in office in accordance with Section 159 (2) of the Companies Act.

BY ORDER OF THE BOARD

J.N. Kimani  
Secretary  
Nairobi  
6<sup>th</sup> October, 1998

**WAKURUGENZI**

Baraza la halmashauri ya wakurugenzi linaonyeshwa kwenye ukurasa wa pili.

Mr D.O. Kombo alijiuzulu mnamo Julai 29, 1997.

Mr F. M. Nyaga aliteuliwa kuwa mkurugenzi mnamo Desemba 17, 1997, na Bi. M.K.Chemengich akajiunga na halmashauri ya wakurugenzi mnamo Machi 13, 1998, kufuatia kuteuliwa kwake kama katibu mkuu wa Wizara ya Fedha kuchukua mahali pa Mr S.S. Lesrima.

Kulingana na agizo 128 ya maagizo ya kampuni, Ms. M.K. Chemengich anajiuzulu, na bado anaruhusiwa, na anajitolea kuchaguliwa tena.

Kulingana na agizo 120 ya maagizo, Mr S.O.J. Ambundo, Mr T.D. Owuor na Mr T.T. Naikuni wanajiuzulu na wakiwa bado wanaruhusiwa, wanajitolea kuchaguliwa tena.

**WAKAGUZI WA HESABU**

Wakaguzi wa hesabu, Deloitte & Touche, baada ya kuonyesha nia, wanaendelea kushikilia wadhifa wao, kulingana na kifungu cha 159 (2) sheria za makampuni.

KWA AMRI YA HALMASHAURI YA WAKURUGENZI.

J.N. Kimani  
Mwandishi  
Nairobi  
Oktoba 6, 1998.

CMA-LIBRARY

We have audited the financial statements on pages 26 to 36 and have obtained all the information and explanations considered necessary for our audit.

The financial statements are the responsibility of the directors. Our responsibility is to express an opinion on the financial statements based on our audit.

We conducted our audit in accordance with generally accepted auditing standards. These standards require that we plan and perform the audit to obtain reasonable assurance as to whether the financial statements are free of material misstatement. An audit includes examining, on a test basis, evidence supporting the amounts and disclosures in the financial statements, assessing the accounting principles used and significant estimates made by the directors, and evaluating the overall financial statement presentation.

In our opinion, proper books of account have been kept by the company and the financial statements, which are in agreement therewith, comply with the Companies Act and give a true and fair view of the company's state of affairs at 30 June 1998 and of its profit and cash flows for the year ended on that date.

Deloitte & Touche  
Auditors  
Certified Public Accountants  
Nairobi  
6<sup>th</sup> October, 1998

Tumekagua ripoti ya fedha ilio katika kurasa za 26 hadi 36 na tumepata habari zote na maelezo yanayohitajika kufanya ukaguzi.

Ripoti ya fedha ni jukumu la wakurugenzi. Jukumu letu ni kutoa maoni kuhusu ripoti hio kulingana na ukaguzi wetu.

Tulifanya ukaguzi wetu kulingana na kanuni zinazokubaliwa za ukaguzi. Kanuni hizo zinahitaji kwamba tupange na tufanye ukaguzi huo tutosheke ya kwamba ripoti za fedha ni kamilifu. Ukaguzi unatia maanani kanuni za hesabu zilizotumiwa, na makadirio ya kifedha yaliofanywa na wakurugenzi, na kuchunguza ripoti ya fedha kwa jumla.

Kwa maoni yetu, kampuni imeweka vitabu vyake vya hesabu vizuri na ripoti za fedha, zinakubaliana na hesabu vyema kulingana na sheria za makampuni na zinaonyesha ukweli kuhusu hali ya kampuni kufikia Juni 30 1998, na mtiririko wake wa faida na pesa kufikia mwisho wa mwaka wa tarehe iliotajwa.

Deloitte & Touche  
Wakaguzi  
Certified Public Accountants  
Nairobi  
Oktoba 6, 1998.

**PROFIT AND LOSS ACCOUNT FOR THE YEAR ENDED 30th JUNE 1998**

**26**

	<b>Note</b>	<b>1998 Sh'000</b>	<b>1997 Sh'000</b>
REVENUE		18,073,232	16,893,149
OPERATING EXPENSES		16,466,480	15,644,324
OPERATING PROFIT	2	<u>1,606,752</u>	<u>1,248,825</u>
EXCHANGE (LOSSES)/GAINS	3	(34,890)	126,702
INTEREST RECEIVABLE	4	590,908	884,749
INTEREST PAYABLE	4	<u>(157,427)</u>	<u>(100,177)</u>
PROFIT BEFORE TAXATION		<u>2,005,343</u>	<u>2,160,099</u>
TAXATION	5	541,068	606,071
PROFIT AFTER TAXATION		<u>1,464,275</u>	<u>1,554,028</u>
DIVIDENDS - GROSS	6	423,946	423,946
RETAINED PROFIT FOR THE YEAR	16	<u>1,040,329</u>	<u>1,130,082</u>
EARNINGS PER ORDINARY STOCK UNIT	7	<u>Sh 27.72</u>	<u>Sh 29.42</u>

	<b>Note</b>	<b>1998 Sh'000</b>	<b>1997 Sh'000</b>
<b>FIXED ASSETS</b>	8	7,548,159	6,587,490
<b>UNQUOTED INVESTMENT</b>	9	4,300	4,300
<b>LOANS RECEIVABLE</b>	10	80,871	146,242
<b>CURRENT ASSETS</b>			
Stocks	11	3,701,006	2,922,129
Debtors	12	8,324,171	6,411,271
Loans receivable	10	80,868	75,670
Short term deposits		958,451	2,634,806
Bank and cash balances		286,682	1,575,794
		<u>13,351,178</u>	<u>13,619,670</u>
<b>CURRENT LIABILITIES</b>			
Creditors	13	11,999,369	12,706,425
Taxation payable		27,996	116,284
Dividends - payable		161,016	178,868
- proposed		263,760	263,760
Loans repayable within one year	17	230,506	226,876
Bank overdraft	14	1,058,063	467,937
		<u>13,740,710</u>	<u>13,960,150</u>
<b>NET CURRENT LIABILITIES</b>		<u>(389,532)</u>	<u>(340,480)</u>
		<u>7,243,798</u>	<u>6,397,552</u>
<b>Financed by:</b>			
<b>SHARE CAPITAL</b>	15	1,098,040	1,098,040
<b>RESERVES</b>	16	4,992,495	3,952,156
<b>SHAREHOLDERS' FUNDS</b>		<u>6,090,525</u>	<u>5,050,196</u>
<b>LOANS</b>	17	1,153,273	1,347,356
		<u>7,243,798</u>	<u>6,397,552</u>

The financial statements on pages 26 to 36 were approved by the board of directors on 6<sup>th</sup> October, 1998, and were signed on its behalf by:

T.T. Naikuni  
S.K. Gichuru } Directors

**CASH FLOW STATEMENT FOR THE YEAR ENDED 30th JUNE 1998**

**28**

	<b>Note</b>	<b>1998 Sh'000</b>	<b>1997 Sh'000</b>
NET CASH (OUTFLOW)/INFLOW FROM OPERATING ACTIVITIES	19(a)	(1,294,654)	2,033,705
RETURNS ON INVESTMENTS AND SERVICING OF FINANCE			
Interest received		672,151	826,920
Interest paid		(166,282)	(106,950)
Dividends paid		(441,798)	(164,861)
NET CASH INFLOW FROM RETURNS ON INVESTMENTS AND SERVICING OF FINANCE		64,071	555,109
TAXATION PAID		(629,356)	(477,722)
INVESTING ACTIVITIES			
Additions to fixed assets, net of capital contributions		(1,542,191)	(2,223,312)
Proceeds from disposal of fixed assets		15,986	25,186
NET CASH OUTFLOW FROM INVESTING ACTIVITIES		(1,526,205)	(2,198,126)
NET CASH OUTFLOW BEFORE FINANCING		(3,386,144)	(87,034)
FINANCING			
Loans received		-	258,019
Repayment of amounts borrowed		(256,427)	(314,949)
Receipt of amount on-lent to KPC		86,978	89,729
NET CASH (OUTFLOW)/ INFLOW FROM FINANCING		(169,449)	32,799
DECREASE IN CASH AND CASH EQUIVALENTS	19(c)	(3,555,593)	(54,235)

## **1 ACCOUNTING POLICIES**

### **BASIS OF ACCOUNTING**

The Company prepares its financial statements on the historical cost basis of accounting.

### **REVENUE**

Revenue represents the total income from the sale of electricity billed during the year excluding Value Added Tax due to the Government.

### **INTEREST**

Interest is accounted for on the accruals basis. Loan interest accruing during the construction of a project is capitalised as part of the cost of the project.

### **STOCKS**

Stocks are valued at average cost less provision for obsolescence.

### **FIXED ASSETS COST**

Additions to transmission lines during the year are capitalised net of customers' contributions.

### **DEPRECIATION**

Depreciation is provided in accordance with the requirements of the Electric Power Act which provides for the write down of the cost of the assets to residual values by equal annual instalments over their estimated useful lives.

### **TAXATION**

Current taxation is provided on the basis of the results for the year as shown in the financial statements, adjusted in accordance with tax legislation.

Deferred taxation is provided on timing differences between the accounting and taxation treatment of certain items of expenditure where, in the opinion of the directors, a significant liability to taxation will crystallise in the foreseeable future.

### **FOREIGN CURRENCIES**

Assets and liabilities denominated in foreign currencies are translated into Kenya Shillings at the rates of exchange ruling at the balance sheet date. Transactions during the year are translated at the rates of exchange ruling at the dates of the transactions. Exchange gains and losses arising during the period of construction of a project are capitalised as part of the cost of the project. Other exchange gains and losses are dealt with in the profit and loss account.

**NOTES TO THE FINANCIAL STATEMENTS (CONTINUED)**

**30**

	<b>1998</b>	<b>1997</b>
	<b>Sh'000</b>	<b>Sh'000</b>
<b>2 OPERATING PROFIT</b>		
The operating profit is arrived at after charging/(crediting):		
Cost of bulk supply:		
Debt service and other operating costs	3,754,872	3,693,175
Power purchases from independent power producers	2,986,815	-
Development surcharge (Note 18)	359,453	1,566,437
Fuel costs	1,794,032	2,083,268
Staff retrenchment costs	192,978	142,430
Directors' emoluments - fees	1,044	1,140
- other	5,639	3,240
Auditors' remuneration	6,050	5,500
Depreciation	579,494	406,484
Profit on disposal of fixed assets	(13,958)	(25,118)
	=====	=====
<b>3 EXCHANGE(LOSSES)/GAINS</b>		
(Loss)/gain on loan capital	(65,974)	140,389
Less: Amount allocated to The Kenya Electricity Generating Company Limited (KenGen)	26,805	(13,687)
	-----	-----
Net exchange (loss)/gain on loan capital	(39,169)	126,702
Exchange gain on prepayments	4,279	-
	-----	-----
Net exchange (loss)/gain for the year	(34,890)	126,702
	=====	=====
<b>4 INTEREST</b>		
Interest receivable:		
On bank and other deposits	590,777	884,317
On deferred capital contributions	131	432
	-----	-----
	590,908	884,749
	=====	=====
Interest payable:		
On loan	52,410	71,065
On bank overdraft	105,017	29,112
	-----	-----
	157,427	100,177
	=====	=====



	<b>1998</b>	<b>1997</b>
	<b>Sh'000</b>	<b>Sh'000</b>
<b>5 TAXATION</b>		
Current taxation		
Based on the adjusted profit for the year at 32.5% (1997-35%)	551,411	554,353
Prior year (overprovision)/underprovision	(10,343)	51,718
	<u>541,068</u>	<u>606,071</u>
	=====	=====

The taxable profit is lower than the profit before taxation mainly due to excess capital allowances over depreciation and the effect of adjusting for realised exchange losses.

#### Deferred taxation

As at 30 June 1998, there was a potential deferred tax liability amounting to Sh 637,000,000 (1997 - Sh 668,599,000).

	<b>1998</b>	<b>1997</b>
	<b>Sh'000</b>	<b>Sh'000</b>
<b>6 DIVIDENDS - GROSS</b>		
Preference stock units	1,930	1,930
Ordinary stock units		
- Interim paid 30 April 1998	158,256	158,256
- Final proposed	263,760	263,760
	<u>423,946</u>	<u>423,946</u>
	=====	=====

#### 7 EARNINGS PER ORDINARY STOCK UNIT

Earnings per ordinary stock unit are calculated on the profit after taxation and preference dividends of Sh 1,462,345,000 (1997 - Sh1,552,098,000) and on the number of stock units in issue at the balance sheet date.

**NOTES TO THE FINANCIAL STATEMENTS (CONTINUED)**

32

**8 FIXED ASSETS**

	Land and buildings Sh'000	Transmission lines Sh'000	Plant and machinery Sh'000	Motor vehicles Sh'000	Furniture, equipment and others Sh'000	Total Sh'000
<b>COST</b>						
At 1 <sup>st</sup> July 1997	948,459	3,749,326	626,214	1,230,303	1,830,042	8,384,344
Additions	52,957	386,230	-	317,531	120,047	876,765
Reclassification	(8,453)	(6,128)	-	(784)	15,365	-
Disposals	-	(378)	-	(17,692)	-	(18,070)
At 30 <sup>th</sup> June 1998	<u>992,963</u>	<u>4,129,050</u>	<u>626,214</u>	<u>1,529,358</u>	<u>1,965,454</u>	<u>9,243,039</u>
<b>DEPRECIATION</b>						
At 1 <sup>st</sup> July 1997	245,351	1,203,287	371,765	598,705	611,244	3,030,352
Charge for the year	40,086	109,461	17,635	181,196	231,116	579,494
Eliminated on disposals	-	(360)	-	(15,682)	-	(16,042)
At 30 <sup>th</sup> June 1998	<u>285,437</u>	<u>1,312,388</u>	<u>389,400</u>	<u>764,219</u>	<u>842,360</u>	<u>3,593,804</u>
<b>NET BOOK VALUE</b>						
At 30 <sup>th</sup> June 1998	<u>707,526</u>	<u>2,816,662</u>	<u>236,814</u>	<u>765,139</u>	<u>1,123,094</u>	<u>5,649,235</u>
Work in progress						<u>1,898,924</u>
						<u>7,548,159</u>
30 <sup>th</sup> June 1997	<u>703,108</u>	<u>2,546,039</u>	<u>254,449</u>	<u>631,598</u>	<u>1,218,798</u>	<u>5,353,992</u>
